

## SALAMU

1. Salamu zenu hakika, hapa zimenifikia,  
Nimeusoma waraka, maelezo yavutia,  
Maombi niliyotaka, yote mumekubalia,  
Muzidi kuendelea, Diwani kuimarika
2. Leo nagamba vigambo, lugha yetu inang'ara,  
Japo kuwa tuko ng'ambo, mila haina hasara,  
Kiswahili si kimombo, kingereza sio bora,  
Asili yetu sitara, ni shina la kila jambo
3. Nawasifu wahariri, wazo lenu la faida,  
Kuchapisha mashairi, katika lenu jarida,  
Mwaonyesha umahiri, bila shaka bila shida,  
Kwetu leo kawaida, twaisoma mistari
4. Hongera ewe Semboja, nawe Aziz Mlima,  
Rushubirwa mupamoja, na yeye Elineema,  
Kalala ninakutaja, Adam kwako lazima,  
Chapisheni tutasoma, beti zitakazo kuja
5. Felix sikusahau, nisalimie Hamza,  
Umwambie angalau, Nkwera amenyamaza,  
Maselle sikudharau, mhariri ulefuzu,  
Tambwe, Madete himiza, muongoze hili dau
6. Hapa nasema tamati, wajibu nami nitunge,  
Mashairi tofauti, kwa ufundi niyapange,  
Nilete kila wakati, nami pia nijiunge,  
Nasimama tuijenge, Diwani ya Tanzaneti

***B. Mwamboga***  
***Holland, 2003***

---